

TOFAUTI YA DHANA YA MWANAMKE KATIKA JAMII: MIFANO KUTOKA KATIKA *TAARAB* (*MIPASHO*) NA NYIMBO ZA KIBENA

ANGELUS MNENUKA

In recent years the question of gender has become so crucial that a related field of studies – known as gender studies- dealing mainly with power relationships between men and women has emerged. The big emphasis for many scholars has been questioning the distribution of responsibilities between men and women. It has been claimed that women have been the victims of oppression and harassment. In other words, the relationship between men and women is not built on equal basis because men benefit more than women while specific roles are assigned depending on the sexes. This paper explores the way these ideas are incorporated in *taarab* music (*mipasho*) and Bena songs sung in a dance called *Mtuli*. I explore the manner in which women responsibilities are discussed meanwhile they reflect distribution of responsibilities/power in the societies that make use of these arts and question the universality of these claims.

Kutokana na tofauti za mazingira, tabia ya nchi na hali ya hewa, binadamu wamekuwa na tamaduni zinazotofautiana na kufanana kwa viwango mbalimbali. Miongoni mwa masuala yanayotofautiana na kufanana ni majukumu yanayofanywa kwa kuzingatia misingi ya jinsi. Kutokana na umuhimu wa suala hilo, kumezaliwa taaluma ya jinsia inayohusu uhusiano uliopo baina ya wanaume na wanawake. Taaluma hiyo inaitwa ujinsia. Kwa miaka ya hivi karibuni msisitizo mkubwa kwa wanataaluma wengi, hasa wanaharakati wanaopigania haki na usawa wa wanawake dhidi ya ukandamizaji unaofanywa na wanaume, umekuwa ukidadi mgawanyo wa majukumu kati ya wanawake na wanaume. Majukumu hayo yameenea karibu katika kila kona ya maisha ya binadamu toka katika siasa, uchumi na majukumu ya kijamii kwa ujumla. Imekuwa ikidaiwa kuwa katika uhusiano baina ya wanawake na wanaume, wanawake wamekuwa wakinyanyaswa na kukandamizwa. Kwa maneno mengine, uhusiano kati ya wanawake na wanaume haujajengwa katika misingi ya usawa kwa sababu wanaume wananufaika zaidi kuliko wanawake. Makala hii inachunguza namna mawazo hayo yanavyosawiriwa katika muziki wa *taarab* (*mipasho*) na nyimbo za ngoma ya Kibena itwayo *Mtuli*. Tunachunguza namna majukumu ya mwanamke yanavyosawiriwa yakidokeza mgawanyo wa majukumu katika jamii zitumiazo sanaa hizo.

Utangulizi¹

Tofauti na watu wengi wasiokuwa na taaluma ya sanaa wanavyofikiri, sanaa haitendeki kwa malengo ya kuburudisha tu, bali inasawiri maisha ya jamii ikiwa ni pamoja na kufafanua mahitaji na changamoto za jamii (Finnegan 1970, 1977, Scheub 1985, Okpewho 1992). Wazo hili linasisitizwa na Okpewho (1992) anapodai kuwa katika jamii asilia za Kiafrika hakukuwa na taasisi za kutolea elimu kama zilivyo hivi sasa, ambapo wanafunzi wengi hujumuika kupata mafunzo kwa kufuata mitaala iliyoandaliwa, badala yake, kazi mbalimbali za sanaa

¹ Makala hii iliwasilishwa kwa mara ya kwanza kwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Orientale kilichopo Napoli nchini Italia. Ninapenda kuwashukuru kwa maswali na maoni niliyopata kutoka kwa mwali-mu wa Kiswahili Dr. Graziella Acquaviva na wanafunzi wa Kiswahili.

zilitumika kutolea mafunzo kwa jamii.² Kwa hiyo, kazi za sanaa zisitazamwe kama burudani tu; ni lazima ziangaliwe kwa kuhusianisha na dhima mbalimbali kulingana na mahitaji na changamoto za jamii itumiayo sanaa hiyo. Karbusicky (1968) anasisitiza kuwa hakuna mtu anayeweza kupinga kuwa kazi mbalimbali za sanaa zinatokana na uhalisia unaotokea katika jamii, na kuwa kazi ya sanaa ina athari kwa jamii. Mawazo hayo yanashadidiwa na Vázquez (1973) anayedai kuwa uhusiano kati ya sanaa na jamii ni mkubwa kwa sababu sanaa ni dhana au tukio la kijamii. Kwa mujibu wa Vázquez (ameshatajwa) sanaa ni dhana au tukio la kijamii kwa sababu msanii mwenyewe ni mwanajamii. Mtalaamu huyu anaendelea kusema kuwa kazi ya sanaa inayohusika pamoja na upekee wake ni kiungo baina ya msanii na jamii inayomzunguka. Aidha, kazi ya sanaa huathiri jamii inayotumia sanaa hiyo kwa sababu sanaa huunga mkono au hukosoa tamaduni za jamii inayohusika, na hakuna mtu anayebaki katika hali yake ya awali baada ya kuguswa na kazi ya sanaa.

Makala hii inalenga kuangalia dhana na nafasi ya mwanamke katika uhusiano wake na mwanamume kijamii na kiuchumi. Mjadala wetu utatalii kwa kifupi majukumu yanayomfasili mwanamke katika jamii kwa kutumia kazi za sanaa kama vile ngoma ya jamii ya Wabena³ iitwayo *Mtuli*⁴ na *mipasho* ambayo ni aina ya muziki wa *taarab* au tawi la *taarab* lililoibuka miaka ya hivi karibuni. Nimeamua kuchambua nyimbo za *Mtuli* na *mipasho* kwa sababu ndizo nyimbo zinazoimbwa hivi sasa katika jamii zinazohusika. *Mtuli* ni ngoma inayochezwa katika sherehe mbalimbali za Kibena hadi hivi sasa wakati makala hii ikiandikwa, hali kadhalika *mipasho* ni muziki ambao unavuma na kutamba katika sehemu za starehe na kumbi mbalimbali, vituo vya redio na televisheni kuliko *taarab* asilia. Makala hii itautazama muziki wa *mipasho* kama muziki unaomwakilisha mwanamke katika tamaduni za jamii mbalimbali zinazoishi maeneo ya pwani ya Afrika Mashariki, hususan jamii za Waswahili. Halikadhalika, makala hii itaitazama ngoma ya *Mtuli* inayodokeza mila na desturi za jamii ya Wabena na mtazamo wao kwa ujumla kuhusu majukumu yanayotarajiwa kutekelezwa na mwanamke katika uhusiano wake na mwanamume kijamii na kiuchumi. Hatuna budi kuyazingatia na

² Ukweli kuwa jamii za Kiafrika hazikuwa na taasisi za kutolea elimu kama ilivyo hivi sasa unapingwa na baadhi ya wataalamu hasa wanapoangalia mifano ya jando na unyago na wakati mwingine madrasa. Ikumbukwe kuwa mafunzo yatolewayo katika jando na unyago yamebanwa katika stadi za maisha kutokana na kuhudhuriwa na vijana wa umri fulani tu, tofauti na taasisi za elimu hivi sasa; kwa hiyo, tofauti kimantiki ipo. Pili, suala la kudai kuwa madrasa zimekuwepo Afrika kwa miaka mingi nalo si la msingi kwa sababu kuwepo kwa madrasa kwa karne nyingi hapa Afrika hakuwezi kufuta ukweli kuwa elimu hii ililetwa na watu kutoka Uarabuni. Na hii inadhihirika katika jamii ambazo Uislamu haukustawi. Mimi pia ninakubaliana na mawazo yaliyotolewa na Okpewho kuhusu uhusiano wa karibu uliopo baina ya elimu na kazi za kifasihi katika jamii nyingi za Kiafrika kabla ya ujio wa wakoloni.

³ Ni jamii ya watu waishio nyanda za juu Kusini mwa Tanzania, hasa katika mkoa wa Njombe. Aidha, Wabena wanapatikana pia katika sehemu ya Kaskazini Magharibi mwa wilaya ya Songea Vijijini, Kaskazini Mashariki mwa wilaya ya Mbeya, sehemu ya Kusini mwa wilaya ya Mufindi, na sehemu ya Kusini Magharibi mwa wilaya ya Ulanga katika mkoa wa Morogoro (Chaula 1989).

⁴ Hii ni ngoma inayochezwa na jamii ya Wabena. Ngoma hii huchezwa kwenye matukio muhimu ya aina tofautitofauti kama vile harusi, sherehe za kijamii, kumbukumbu ya marehemu ambayo kwa kawaida hufanyika mwaka mmoja baada ya mtu mzima kufariki dunia. Kumbukumbu hiyo inaweza kurudiwa mara kadhaa kulingana na uamuzi wa anayehandaa tukio hilo.

TOFAUTI YA DHANA YA MWANAMKE

kuyatilia maanani maneno na dhana zinazoimbwa katika sanaa hizi kwa sababu zinaakisi mila na desturi za jamii zinazotumia sanaa hizo.

Nyimbo zitakazotumika katika makala hii ni zile tu zenye uhusiano wa moja kwa moja na masuala yanayogusa majukumu au nafasi ya mwanamke katika jamii kwa sababu msingi mkuu wa mada yetu ni jinsia. Hata hivyo, makala hii itaangalia kwa namna ya pekee uhusiano kati ya mwanamke na mwanamume katika jamii na namna mgawanyo wa majukumu unavyohusishwa moja kwa moja na jinsi, yaani ujinsia. Tunataka kuangalia uhusiano huu katika suala zima linalohusisha kuishi pamoja kati ya mwanamke na mwanamume bila kujali kama wanaishi katika ndoa rasmi au wanaishi kihawara. Tunatarajia nyimbo zitakazotumika zitadokeza mgawanyo wa majukumu ya mwanamke na mwanamume katika jamii zitumiazo sanaa zinazojadiliwa.

Kabla ya kuanza kuchambua baadhi ya nyimbo za *mipasho* hatuna budi kuweka bayana kwa kifupi tofauti ya dhana za *taarab* na *mipasho* kwa sababu dhana hizi mbili zinaelekea kuwakanganya wengi hasa wale wasiouelewa barabara muziki huu. Neno “*mipasho*” linatokana na kitenzi cha lugha ya Kiswahili “pasha”⁵ likiwa na maana ya kusema kitu bila kuficha chochote. Hatuwezi kuikubali maana ya neno “kupasha” iliyotolewa na Beez na Kolbusa (2003:54) kuwa ni “kumfanya mtu apate” au “kuteta” kwa sababu, kimantiki haiwezekani kumteta mtu kwa kutumia nafsi ya pili.⁶ Wazo hili linathibitishwa na mtunzi wa nyimbo za *taarab* aitwaye Haji Machano anayesema,

[Nyimbo] za sasa ni very transparent, wazi, zamani walikuwa wanaficha wanatumia nyimbo za mafumbo. Akisema analipenda tunda, analipenda, analihusudu, analisifu tunda anavyolipenda kumbe sio tunda ni mtu. Lakini siku hizi huwezi kusifu tunda unamwambia yule mtu mwenyewe moja kwa moja nakupenda nakutaka, I need you, I love you na vitu kama hivyo. Lakini zamani unatumia vitu kama ndege, ndege hawa birds. Unaweza kumsifu ndege wako vile anavyoruka na kutua na vipi kumbe unamsifu mtu. Sasa kikubwa nilichokigundua mimi ni kwamba zamani walikuwa wanaficha walikuwa wanatumia lugha ya sitiari. Lakini siku hizi wanaweka wazi wazi kuelezea kila kitu. (Traoré 2004: 79)

Kwa bahati mbaya, pamoja na utamaduni wa Waswahili wa kutumia misemo yenye mafumbo hata katika matukio ya kuelezana ukweli, muziki wa *mipasho* umeenda mbali zaidi na

⁵ Kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (TUKI 2004) na *Kamusi la Kiswahili Fasaha* (BAKIZA 2010), neno hili linamaanisha kutoa taarifa, lakini watumiaji wa Kiswahili hulumia neno hili pia kwa maana ya kumweleza mtu ukweli bila kuficha chochote ikiwa ni pamoja na kutotumia lugha ya mafumbo. Maana hii, ambayo haijafanuliwa katika kamusi zote mbili zilizotajwa hapo juu ndiyo iliyotumika kuunda neno “*mipasho*” dhana inayoutambulisha aina ya muziki uliochepuka kutoka katika *taarab*.

⁶ Dhana ya “kumfanya mtu apate” kama ilivyoandikwa kwa lugha ya Kiingereza “cause somebody to get” ni ya kiisimu zaidi ambayo haina mchango mkubwa katika makala hii. Dhana yenye matatizo na inayoweza kupotosha ni kudai kuwa “kupasha” ni “kuteta” yaani “backbite” kwa lugha ya Kiingereza, hatuwezi kukubaliana nayo kwa sababu kuteta ni kuzungumza masuala yanayomhusu mtu kwa nia isiyo njema bila yeye kuwepo. Ikiwa kumpasha mtu ni kumzungumzia mtu asiyekuwepo, basi *mipasho* ingehusisha nafsi ya tatu badala ya nafsi ya pili. Nafsi ya pili inatusaidia kujua kuwa watu wanaogombana wanasemana moja kwa moja na sio vinginevyo. Kimsingi hiyo ndiyo maana halisi ya neno “kupasha” kama linavyotumiwa katika mawasilino ya lugha ya Kiswahili wakati makala hii ikiandikwa.

kukiuka taratibu za kawaida za Mswahili kwa kueleza dhana zake waziwazi, kwa kutumia, wakati mwingine, lugha isiyo na staha wala tasifida. Ingawa baadhi ya wataalamu hudai kuwa kwa asili yake sanaa hukiuka kaida na msingi wa ujumi wa kisanaa kutokana na ukiushi wa kikaida (Karbusicky 1968); ukiushi unaojitokeza katika *mipasho* hauelekei kukiuka kaida kwa malengo ya kisanaa tu, bali inawezekana kuwa matumizi ya lugha ya mafumbo na utunzi wa sitiari na misemo mbalimbali imepungua kutokana na, ama haraka ya kutoa nyimbo kwa malengo ya kibiashara kama ilivyodokezwa na Khamis (2002), au ujuzi mdogo wa kutumia sitiari na mafumbo kwa ujumla katika tungo zao.⁷

Baadhi ya sifa za muziki wa *mipasho* ni mashairi yake kutobanwa kwa kanuni ya urari wa vina na mizani. Halikadhalika, vifaa vya muziki vinavyotumika pamoja na mahadhi ya *mipasho* ni tofauti kwa sababu *taarab* inatumia vifaa vingi ilhali *mipasho* hutumia vifaa vichache na kufuata mtindo wa muziki wa dansi wa Kilingala, yote haya yakishinikizwa na uhitaji wa kuingiza muziki sokoni mapema (Kirkegaard 2002, Khamis 2002, 2004, 2005). Muziki wa *taarab* umeenea katika maeneo mbalimbali kama vile Msumbiji, Afrika Mashariki, eneo la Maziwa Makuu ikiwa ni pamoja na Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Afrika ya Kaskazini na Uarabuni.⁸ Mafumbo yanayotumika katika muziki wa *taarab* ni magumu kufumbuliwa na wenyeji wa waishio maeneo ya bara wasio na ufahamu wa kutosha wa muziki huu na hasa zaidi utamaduni wa Waswahili. *Mipasho* imerahisisha kwa kiwango kikubwa kuelewa dhambi na masuala mbalimbali yanayotumiwa katika *taarab* kwa sababu lugha ya picha, sitiari na mafumbo yaliyotumiwa katika *taarab* asilia si rahisi kufumbuliwa hasa na watu wa bara kwa sababu mbalimbali, kubwa zikiwa ni za kimazingira na kitamaduni. Makala hii itajadili mtazamo na mawazo yanayopatikana katika *mipasho* yakihusishwa na jamii zinazoishi maeneo ya pwani ya Tanzania hususan Dar es Saaam, Tanga na Zanzibar: jamii zinazopatikana katika maeneo ya pwani ya Afrika Mashariki zimekaribiana sana kijiografia, kitamaduni, na vilevile zina historia ya kutumia muziki wa *taarab* kwa muda mrefu ikilinganishwa na maeneo mengi ya bara.

Dhana ya mwanamke katika ngoma ya *Mtuli*

Dhana ya mwanamke katika *Mtuli* ni kiwakilishi cha mtazamo wa Wabena kwa ujumla kwa sababu sanaa ni zao la jamii na moja ya dhima zake ni kuonyesha masuala mbalimbali katika jamii ikiwa ni pamoja na changamoto za kimaisha kwa ujumla. Ili sanaa ikubalike katika jamii ni lazima iakisi mawazo na changamoto za jamii inayohusika. *Mtuli* ni ngoma inayotumi-

⁷ Inawezekana kuwa ukiushi wa kikaida unaojitokeza katika nyimbo za *mipasho* unachangiwa pia na ukweli kuwa muziki huu unavuka mipaka ya jamii ya Waswahili na hivi sasa kuimbwa na kutumiwa na watu kutoka katika jamii nyingine ambazo lugha na utamaduni vya Kiswahili havijakita mizizi yake barabara. Hata hivyo, athari hii ni ndogo sana kwa sababu *mipasho* ilianza miaka mingi iliyopita huko Zanzibar kabla ya kupata umarufu mkubwa Tanzania bara ambako kuna jamii nyingi zisizoujua vema utamaduni wa Waswahili (rejea Traoré, 2007).

⁸ Hayo ni baadhi ya maeneo yaliyotajwa na Igobwa (2007) akimrejelea Khamis (2005).

TOFAUTI YA DHANA YA MWANAMKE

ka katika matukio muhimu katika jamii; bila shaka ni ngoma iliyosheheni utamaduni, mila na desturi za Wabena ikibeba kwa kiwango kikubwa mtazamo wao wa ulimwengu (ontolojia). Hata hivyo, hatupaswi kusahau kuwa jamii ya Kibena inabadilika na kwamba si kila Mbena popote alipo anafuata mila na desturi hizi, lakini idadi kubwa ya jamii asilia za Kibena hu-fuata mila na desturi za Kibena. Kwa hiyo, hatuna budi kuzichukulia nyimbo hizo kama kiwa-kilishi cha mila na desturi za jamii asilia ya Kibena.⁹

Mwanamke kama mfanyakazi

Pamoja na sifa mbalimbali alizonazo mwanamke katika jamii ya Kibena, kufanya kazi ni sifa kubwa na yenye hadhi ya juu miongoni mwa wasichana wanaotaka kuolewa. Ni muhimu kwa mwanamke kuwa na bidii katika kazi kwa sababu mara baada ya kuolewa, yeye (mwanamke) na mumewe wanapaswa kujitegemea. Kujitegemea huko kunaongezeka zaidi ikiwa mwanamke huyo ameolewa katika ndoa ya ukewenza, au ameingia katika ukewenza baada ya mume-we kuamua kuoa mwanamke mwingine. Suala la mitara ni la kawaida katika utamaduni wa Wabena, kama ilivyo katika jamii nyingi za Kibantu (Mbiti 1969, Magesa 1998). Hivyo, ili mwanamke amudu maisha yake, hana budi kujibidisha katika kazi. Katika jamii asilia ya Kibena, wazazi na ndugu humsaidia mtoto wao wa kiume kumchagua msichana mwenye bidii ya kazi ili nyumba yao isije kuishiwa chakula, suala linalotia aibu katika familia nzima. Kwa hiyo, mwanamke ni msingi na nguzo imara ya kuitegemeza kaya. Wazo hili linajitokeza kati-ka nyimbo nyingi za ngoma ya *Mtuli*. Hapa tutatoa mfano mmoja wa wimbo uitwao *Ligimilo*:

Iligimilo

iligimilo ni nyengo, ye dado nu nyoko,

iligimilo ni nyengo, ye dado nu nyoko.

ukangalage ulimage, ulalya kumwaka,
ukangalage ulimage, ulalya kumwaka.

Jembe

jembe na nyengo,¹⁰ ni baba na
mama yako,

jembe na nyengo, ni baba na
mama yako.

kazana kulima utakula mwakani,
kazana kulima utakula mwakani.

Ubeti huo una maneno ambayo hutumika kumuasa mwanamke; ingawa haujataja bayana ana-yeambiwa, lakini kulingana na muktadha wa jamii ya Wabena, mvulana anayefikia hatua ya kuoa ni lazima awe na uwezo wa kujitegemea na wakati mwingine kutoa msaada kwa ndugu na hasa wazazi, walezi na ndugu wa karibu. Kutokana na ukweli huo, maneno hayo yanaele-kezwa moja kwa moja kwa mwanandoa wa kike ambaye kwa muda wote kabla ya kuolewa alikuwa chini ya wazazi wake, na wakati mwingine aliwategemea kwa kiasi kikubwa. Wimbo huo unadokeza kuwa jukumu la kufanya kazi kwa mwanamke katika jamii ya Kibena linaanza rasmi baada ya kuolewa ambapo hana nafasi ya kumtegemea mtu mwingine katika maisha

⁹ Pamoja na ukongwe wake, nyimbo za Kibena bado ni hai na ni vigumu sana kuona sherehe yoyote ile ya Kibe-na isiyotumbuzwa na nyimbo hizo za Kibena katika mkoa wa Njombe walimo Wabena na maeneo mengine.

¹⁰ Hiki ni kifaa chenye mpini unaofanana na mpini wa jembe unaochomekewa kitu kama kisu kikubwa kitumi-wacho na Wabena na jamii zingine ziishizo maeneo hayo kwa ajili ya kufyekea nyasi na miti midogomidogo.

ANGELUS MNENUKA

yake ya kila siku. Uvivu ni sifa mbaya sana miongoni mwa wanawake wa Kibena kiasi cha kuwa miongoni mwa sababu za msingi zinazoweza kuhalalisha mwanamke kupewa talaka (Culwick & Culwick 1935).¹¹

Katika ubeti mwingine wa wimbo huu kuna mistari ifuatayo: “*Thodihodi mukilawo, twivelye tulema,*” “*Ipetupetu mukilawo Twivelye tulema*” yakimaanisha, “Kupigapiga hodi asubuhi (kwenye nyumba za watu kuomba chakula), hatutaki,” “Kuombaomba chakula asubuhi (kwenye nyumba za watu), hatutaki.” Maneno hayo yanakemea tabia ya kuomba chakula katika kaya zingine asubuhi kwa sababu hicho ni kitendo kinachotia aibu. Kisha waimbaji huitikia kama ifuatavyo: kazana kulima, utavuna mwakani, wakisisitiza umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii. Wazo hili linaweza kuelekezwa vizuri zaidi baada ya kuchunguza ubeti wa wimbo unaofuata hapo chini ambao unatupeleka kwenye hoja nyingine inayodokeza kuwa ndoa si lelemama.

Nafasi ya mwanamke katika ndoa

Kulingana na mahitaji ya kimaumbile na kitamaduni, watu wengi katika jamii mbalimbali duniani wana mwelekeo wa kuoa na kuolewa. Ni suala la kawaida kuona baada ya msichana na mvulana kufikia umri fulani huhitaji kuishi na mwenzi au wenzi katika baadhi ya jamii. Katika jamii ya Kibena, ndoa kwa msichana si kitu cha kukichukulia juujuu au kimzahamzaha kwa sababu ndoa inamtaka mwanamke kukabili majukumu makubwa pengine zaidi ya yale aliyoyazoea katika kaya aliyokulia, yaani kwa wazazi au walezi wake. Baadhi ya majukumu makubwa ni kufanya kazi kwa bidii, na kuhakikisha kuwa watoto, kama wapo, wanatunzwa na kulelewa vizuri kulingana na mila na desturi za jamii. Kutokana na majukumu hayo, ambayo wakati mwingine hutekelezwa bila usaidizi kutoka kwa mwanamume, na kutokana na kuzidiwa na majukumu, aghalabu mwanamke hujikuta akipoteza uzuri aliokuwa nao kabla ya kuolewa. Wimbo ufuatao, kama tulivyosema hapo juu, unaunganisha wazo la mwanamke kufanya kazi na kupoteza uzuri wake.

Iminamina

*iminamina umwana ali pa ng'ina,
iminamina umwana ali pa ng'ina,
vwone atawuke umwana isweleluka,
vwone atawuke umwana isweleluka.*

Anadeka

mtoto hudeka akiwa kwa mama yake,
mtoto hudeka akiwa kwa mama yake,
lakini mtoto akiolewa huchakaa,
lakini mtoto akiolewa huchakaa.

Ubeti huo unadokeza wazo la msichana kufurahia maisha kabla ya kuolewa ambapo mahitaji au changamoto kubwa za kimajukumu huwa chini ya wazazi wake, matatizo yoyote yanayoweza kumtokea yanaweza kutatuliwa kwa msaada wa wazazi wake huku yeye akishiriki au akiwa kando. Inawezekana pia maneno ya wimbo huo yanamaanisha kuwa kabla ya kuolewa,

¹¹ Ingawa wataalamu hawa wanazungumzia Wabena waishio maeneo ya Morogoro, tunaamini kuwa, pamoja na tofauti kadha wa kadha zinazoweza kujitokeza baina ya Wabena wa nyanda za chini na wale wa nyanda za juu, bado kuna masuala mengi ya msingi ya kimila yanayowaunganisha.

TOFAUTI YA DHANA YA MWANAMKE

msichana huwa na uhuru mkubwa; anaweza kuamua ale nini, ale saa ngapi, afanye nini, aende wapi kulingana na matakwa yake huku akifuata mila na desturi za jamii ya Kibena.¹² Uhuru ambao baada ya kuolewa hutoweka kutokana na kuwa chini ya mume, lakini zaidi ni kutokana na kuzidiwa na majukumu kiasi cha kuanza kupoteza uzuri wa usichana wake. Ndiyo maa-na tunapenda kusisitiza tena kuwa juhudi katika kazi kwa mwanamke wa Kibena ni silaha kubwa inayomwezesha kumudu maisha. Kwa hiyo, ndoa si kitu au si taasisi ya kuikimbilia bila kujiandaa vizuri. Vilevile, tahadhari inatolewa kwa wasichana kuwa mwanamume si mtu wa kumkimbilia na kupenda kuishi naye bila kujiandaa namna ya kuishi naye.

Mwanamke kama mtu anayenyanyaswa katika jamii

Katika kufanya kazi kwa bidii, juhudi na maarifa, na kutimiza majukumu mbalimbali, katika mazingira fulani, mwanamke hunyanyaswa kimfumo. Suala hili la unyanyasaji kwa wanawake si geni katika jamii ya Kibena. Mama na ndugu wa msichana anayeolewa huyaona haya na kamwe hawakubaliani nayo. Kwa sababu hiyo, ndugu wa karibu wa mwanamke hushiriki katika kutoa uamuzi kuhusu mwanamume anayetaka kumwoa msichana. Pamoja na mambo mengine, ndugu na jamaa wa karibu wa msichana huchunguza tabia na mwenendo wa mwanamume, ikiwa ni pamoja na bidii yake katika kazi. Ikiwa mwenendo wake ni wa kuridhisha, ndipo hukubaliwa kumwoa msichana. Pamoja na hayo yote, unyanyasaji huendelea kutokea kwa sababu mbalimbali. Wazo hili tunalipata katika wimbo ufuatao:

Ali yuyo

*ali yuyo, ali yuyo, ali yuyo, ali yuyo,
ali yuyo mwana visu ali yuyo.*

Huyo ni mtoto pekee

huyo ni mtoto pekee,
huyo ni mtoto pekee tuliyenaye.

Ubeti huu una maneno yanayotolewa na mzazi au ndugu wa msichana anayeolewa, wakimweleza mwanamume anayeoa msichana kuwa katika familia anayotoka msichana kuna mtoto mmoja tu au msichana mmoja tu; na mtoto huyo ndiye anayeolewa. Wimbo huu una mawazo kadhaa yaliyofumbatwa.¹³ Baadhi ya mawazo hayo ni tahadhari kwa mwanamume anayeoa kuwa mwangalifu asimfanyie vitendo vya unyanyasaji mke wake kwa kuwa ni mtoto pekee katika familia. Wazazi na ndugu wanamkanya mwanamume huyo kuwa asidiriki kufanya vitendo vya unyanyasaji kwa mke wake kwa sababu, ikiwa msichana huyo atapata matatizo yoyote ya ulemavu au kufariki dunia, ajue kuwa atakuwa ametia doa kubwa katika familia ya msichana huyo. Kwa kifupi, wimbo huu unasisitiza kuwa wanaume wasifanye vitendo vya unyanyasaji kwa wake zao, wazo linalodokeza kuwa kuna vitendo vya unyanyasaji kwa wa-

¹² Pamoja na kukabiliwa na majukumu kadha wa kadha, msichana ambaye anaishi kwa wazazi wake katika jamii ya Kibena ana uhuru zaidi kuliko yule aliyeolewa. Kwa mfano, msichana anayeishi kwa wazazi wake anaweza kuamua kwenda kwenye ngoma au kuwatembelea ndugu na kukaa huko siku kadhaa kulingana na matakwa yake, lakini mwanamke aliyeolewa ni lazima apate ruhusa ya kufanya hivyo kutoka kwa mume wake.

¹³ Kulingana na mahojiano na baadhi ya Wabena, maana nyingine ya wimbo huu ni mtoto wa pekee, yaani mto-to mwenye nafasi ya pekee katika familia kama vile mtoto anayetegemewa kwa ushauri au nguvukazi.

ANGELUS MNENUKA

nawake katika jamii ya Kibena. Hata hivyo, unyanyasaji kama vile kupigwa na mumewe ukizidi mwanamke anaweza kuomba talaka (Culwick & Culwick, wameshatajwa).

Mwanamke kama mzazi

Kutokana na majukumu makubwa aliyonayo katika kufanya kazi, mwanamke anahitaji watoto wenye afya watakaomsaidia kufanya kazi. Vilevile, watoto watamsaidia mama huyo baada ya kuzeeka. Kutokana na hilo, watoto wana umuhimu mkubwa katika kaya za Kibena kwa madhumuni hayo na mengine ya kiontolojia. Watoto wa ndugu wa karibu wanaweza kuishi pamoja na mwanamke huyu ambaye wakati mwingine hana watoto ili kumsaidia kazi. Kutokana na suala la watoto kuwa nyeti, mwanamke asiye na watoto huhuzunika na kufadhaika kwa kiwango kikubwa sana. Suala hilo linajitokeza katika wimbo ufuatao:

*Ede*¹⁴

nde mgayu mwana ndiguda nange nange (2)

*nde mkiva nene ndiguda, nange nange,
ndongela nani ndiguda nange, nange,*

ndongela nani ani ve, nange, nange.

Ede

mimi sina mtoto
nahangaika, nisaidie (2)
mimi ni mkiwa, nisaidie,
nitazungumza na nani
nahangaika, nisaidie,
nitazungumza na nani, nani
jamani, nisaidie.

Maneno hayo ni sehemu ya wimbo unaozungumzia matatizo ya kukosa mtoto aliyonayo mwanamke. Mwanamke anasikitika kukosa mtoto kwa sababu za kijamii, kiuchumi na kiontolojia. Kwa hiyo, tunaweza kusema kuwa na mtoto ni moja ya nguzo kuu katika kaya katika jamii ya Kibena. Kitendo cha mwanamume kuwa na watoto wengi kwa wake mbalimbali ni moja ya sifa kubwa. Kwa hiyo, nafasi ya mwanamke kama mzazi ni suala muhimu na lenye upekee mkubwa kwa sababu kutokuwa na uwezo wa kuzaa ni sababu kubwa inayohalalisha mwanamume kuoja mwanamke mwingine hata kama nafsi yake haimtumi kufanya hivyo (Mbiti 1969).

Mwanamke kama mlezi

Haitoshi kwa mwanamke kuwa na watoto, kwani watoto wanapaswa kulelewa katika misingi yenye kuzingatia mila na desturi za jamii ya Kibena. Mwanamke kama mzazi anapaswa kuha-kikisha kuwa watoto wanalelewa kulingana na mila na desturi za jamii inayohusika. Kwa kawaida, tabia mbaya aliyonayo mtoto inatokana na malezi mabaya aliyoyapata kutoka kwa mama yake kwa sababu mama huwa karibu na mtoto kwa muda mrefu. Suala hili ni muhimu

¹⁴ Wimbo huu huimbwa na jamii za Wabena na Wahehe katika matukio ya harusi na mengine yanayofanana na hayo, lakini mapigo, maneno na sifa zingine za kiisimu vinaonesha kuwa wimbo huu una asili ya Kihehe zaidi kuliko Kibena. Hata hivyo, umetumika katika makala hii kwa sababu ni wimbo unaoimbwa katika jamii ya Wabena. Kukubalika na kuimbwa katika jamii ya Wabena kunamaanisha kuwa wimbo huo unaakisi mila na desturi za Kibena pia. Aidha, jamii za Kibena na Kihehe zinafanana kwa kiasi kikubwa katika masuala ya msingi ya kitamaduni na kilugha (Mumford 1934).

TOFAUTI YA DHANA YA MWANAMKE

kuzingatiwa kwa sababu kwenye ndoa za ukewenza, ambapo mwanamume ana mke zaidi ya mmoja, jukumu la kuwalea na kuwafunza watoto tabia njema linawahusu wanawake moja kwa moja kwa sababu mwanamume ambaye ni baba wa watoto hana ratiba maalumu ya kuonekana nyumbani, anaweza kurudi au kutorudi. Kwa hiyo, mama wa watoto ndiye anayewajibika kwa kiasi kikubwa. Wazo linalosisitiza umuhimu wa malezi kwa watoto linajitokeza katika wimbo ufuatao.

Mama pagate umwana

*mama upagate umwana pe ivemba,
mama upagate umwana pe ivemba,
mama upagate umwana pe ivemba,
mama upagate umwana pe ivemba.*

Pakata mtoto

mama mpakate mtoto anapolia.

Wimbo unasisitiza umuhimu wa malezi kwa mtoto. Wimbo huu umetumia lugha ya picha kwa kiasi kikubwa kwa sababu dhana ya kupakata mtoto haipaswi kuangaliwa katika mipaka ya kumshika mtoto mikononi tu. Wazo la kumpakata mtoto ni kumlea na kumtunza ili aishi kwa amani. Dhana ya kutokulia inabeba wazo la kutulia na kuwa na amani, yaani kuishi kulingana na mila na desturi za jamii ya Wabena. Kulia ni kuwa na matatizo ambayo yanamfanya mtoto mwenyewe kutokuwa katika hali ya amani na utulivu. Halikadhalika, kulia ni kuwa na matatizo yanayowakera wanajamii wengine hasa ndugu na jamaa wa karibu kiukoo kwa kuwatia aibu na kuwadhalilisha kutokana na tatizo la kutopakatwa, yaani kutolelewa katika maadili mazuri. Mtoto anaweza kulia kwa sababu ya njaa, maana yake anahitaji chakula. Hivyo, mwanamke kama mzazi anapaswa pia kuhakikisha kuwa hakuna tatizo la njaa katika kaya yake. Inawezekana pia mtoto akalia kwa sababu haheshimiwi katika jamii kutokana na malezi mabaya aliyopata kwa wazazi wake (Mnenuka 2009). Kwa hiyo, pamoja na ndugu, watoto wenye umri mkubwa na mama mzazi mwenyewe, wote kwa pamoja wana jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa mtoto analelewa kulingana na mila na desturi za jamii.

Kwa kifupi, nafasi ya mwanamke katika jamii ya Kibena inasawiriwa barabara na nyimbo hizo ambazo huimbwa katika matukio ya harusi zikiwa na malengo ya kuburudisha na hasa kufikisha ujumbe muhimu kwa mwanamke ili ajue wajibu na majukumu yanayotarajiwa kufanywa na yeye kama mwanamke katika jamii. Wajibu na majukumu hayo huweza kutofautiana toka familia moja hadi nyingine kulingana na nafasi ya mwanamume au utashi wa mwanamume aliyeoa, ingawa tofauti ndogondogo zinazoonekana haziwezi kuondoa mfumo unaoweka bayana majukumu ya mwanamke katika jamii hiyo.

3 Dhana ya mwanamke katika *mipasho*

Kwa mujibu wa Khamis (2002), dhamira mbalimbali zinazojadiliwa na wasanii wa *mipasho* si ngeni; ni dhamira ambazo zimekuwa zikijadiliwa miaka mingi katika muziki wa *taarab*. Tofauti kubwa inayojitokeza katika *mipasho* ni lugha inayotumika. Khamis (ameshatajwa) anaendelea kusema kuwa katika *taarab*, masuala mbalimbali yalijadiliwa kwa lugha ya mafumbo, ikiwa ni pamoja na kutotamka baadhi ya maneno hadharani; lakini suala hilo linaji-

ANGELUS MNENUKA

tokeza kwa kiwango kidogo sana katika muziki wa *mipasho*. Muziki wa *mipasho* unaakisi kwa kiasi kikubwa mila na desturi za jamii ya watu wa pwani, hata kama unaimbwa katika maeneo mbalimbali ya bara kama tulivyokwishaona hapo juu.

Mwanamke kama mrembo

Uzuri ni suala muhimu kwa mwanamke na ni silaha muhimu katika mapambano ya kumpata mwanamume. Mwanamke mzuri anaweza kumshawishi kapera au mume wa mtu. Baada ya kufanikiwa kumteka mwanamume, uhusiano kati ya mwanamke na mwanamume unaweza kuwa wa kihawara au unaweza kuimarika zaidi na kuwa ndoa rasmi. Vigezo vikubwa vya uzuri vinavyozingatiwa katika *mipasho* ni maumbile, urembo na mavazi. Kwa kawaida mwanamume anayelengwa ni yule mwenye sifa mbalimbali kama vile mwenye mali, mwenye umaarufu au sifa zingine zinazomvutia mwanamke. Kazi kubwa aliyonayo mwanamke ni kuhakikisha kuwa uzuri huo unatunzwa ili awe na nguvu na uwezo wa kumshindania mwanamume. Ubeti ufuatao wa wimbo wa *Kubali Matokeo* uliotungwa na Khadija Kopa unadokeza wazo hilo la uzuri na umuhimu wake kwa mwanamke.

Kubali matokeo

mwanamke nyonga (2)
mwanamke kutingishika, kushikwa akashikika,
mwanamke kuitika, bwana anapomwita,
mwanamke kuvikata, kata kata,
mwanamke ninavikata, kata kata,
mwanamke nyonga, makalio majaliwa.

Wimbo huo unaonyesha wazo la uzuri kuwa ni suala la kujivunia katika haratakati za kushindania wanaume, na ni suala linalojitokeza katika nyimbo nyingi za *taarab* (Beez na Kolbusa, wameshatajwa). Kwa hiyo, uzuri kwa mwanamke ni silaha muhimu katika maisha ili kufanikiwa kuolewa. Katika mwelekeo huo wa majigambo, wanawake husutana na hutukanana kwa kutumia kigezo hicho cha uzuri. Ubeti ufuatao uliodondolewa kutoka wimbo wa *Kiwango* uliotungwa na Asmahani Saidi unadokeza wazo la kushutumiana na kutoleana tambo zinazonyesha kuwa uzuri ni kigezo muhimu kwa mwanamke.

Kiwango

niangalie nilivyo, mie nawe hatuko sawa,
mwanamke hovyohovy, huna anapovutia,
mapenzi yako mchovy, dhahabu iliyoibiwa,
hujulikani ulivyo, si kiuno si kifua,
bibi huzijui tungo, chumvi unalia miwa,
kengeza waita chongo, hujui ilivyozaliwa,
mambo yote kwa kiwango, bibie ushaupwelea.

Kuna nyimbo nyingi za aina hii katika muziki wa *mipasho* zenye majigambo yanayodokeza wazo la uzuri kuwa silaha muhimu katika mashindano ya kumpata mwanamume.

TOFAUTI YA DHANA YA MWANAMKE

Ujuzi wa mbinu za ushawishi

Pamoja na uzuri, mwanamke anapaswa kuwa na mbinu za ushawishi zinazomsaidia kumdhibiti mwanamume asiende kwa wanawake wengine. Mbinu hizo hutofautiana kutoka mtu mmoja hadi mwingine. Ujuzi na uwezo wa mbinu hizi huweza kumfanya mwanamume amwache mke wake na aoe mwanamke mwenye ushawishi zaidi, au mwanamume anaweza kuoia mke mwingine mwenye ushawishi zaidi bila kumwacha mkewe wa awali. Hali hii huchangia kuleta msuguanu kati ya wake tofauti wa mume mmoja. Kutokana na hali hii, suala la ushawishi halipaswi kwisha miongoni mwa wake waliolewa na mume mmoja; ni suala endelevu, kwa sababu ushawishi unapolegalega humfanya mwanamume aende kwa wanawake wenye ushawishi zaidi. Kimsingi, hali hii ya ushawishi huwaleta pamoja wanawake wenye umri mkubwa na wasichana katika uwanja mmoja wa mashindano. Baadhi ya maeneo yanayojadiliwa kuwa na ushawishi miongoni mwa vitu vingine vingi ni namna ya kumliwaza mwanamume, usafi, tabia njema na ubobezi katika mahaba. Vitu hivyo humfanya mwanamume ampende na kuishi na mwanamke; amwache au amwoe mwanamke mwingine.

Ubeti ufuatao wa wimbo wa *Vijimambo* ulioimbwa na kikundi cha *Dar Modern Taarab* unaonyesha wazo hilo la kumliwaza mwanamume kama nyenzo muhimu ya kuimarisha uhusiano kati ya mwanamke na mwanamume.

Vijimambo

kwanza mwanamke nyonga, siri hiyo ubaini,
pili ujue kuringa, wanawake wa chumbani,
mvalie moja kanga, unapotoka bafuni,
kisha, mshike mabega, mbusubusu shavuni *dear*,
akikupapasa nyonga, nenda naye uwanjani habibi,
kisha, mshike mabega, mbusubusu shavuni *dear*,
akikupapasa nyonga, nenda naye uwanjani habibi,
mwenzangu yamekushinda, hayo kuyabaini,
ndipo mi nimemsomba, bwana nimemweka ndani,
mwenzangu yamekushinda, hayo kuyabaini,
ndipo mi nimemsomba, dear nimemweka ndani,
mpenzi nimemviringa, nimemtia kwapani,
namzungushia nyonga, spidi mia tisini.
mpenzi nimemviringa, nimemtia kwapani,
namzungushia nyonga, spidi mia tisini.

Wimbo huu unaonyesha namna mwanamke anavyotoa huduma mbalimbali kwa mwanamume ili amshawishi, aridhike na asiende kwa mwanamke mwingine. Pamoja na wazo hilo la kumliwaza mwanamume, wimbo huu unaonyesha kuwa mwanamume anayezungumziwa alikuwa mume au hawara wa mwanamke mwingine ambaye hivi sasa ndiye anayeambiwa. Tunaona baadhi ya masuala muhimu anayofanyiwa mwanamume ili aliwazike na aendelee kumpenda mwanamke huyu na wala asitamani kwenda kwa mwanamke mwingine. Masuala yanayojitokeza katika wimbo huu ni kama vile namna ya uvaaji wa nguo, uwe ni uvaaji unaoamsha ashiki. Aidha, msanii anaendelea kufafanua mbinu zingine nyingi ambazo ni muhimu katika kuimarisha uhusiano kati ya mwanamke na mwanamume. Baadhi ya madondoo kutoka katika

ANGELUS MNENUKA

beti tofauti za wimbo wa *Utalijua Jiji* ulioimbwa na kikundi cha *East African Melody* yanaonyesha mwanamke asiyewajibika anaweza kumpoteza mwanamume kwa sababu wanawake wengine wana ushawishi zaidi. Kwa hiyo, athari kubwa ya mwanamke asiyewajibika ni kutelekezwa au kuachwa na mwanamume ambaye kimsingi ndiye nguzo yake kimaisha, yaani anayemtegemea kwa kila kitu.

Utalijua jiji

mwenzangu huna ujuzi, mpenzi umemuudhi,
kaja kwangu nimempokea, kaja kwangu nimempokea,
hata ukinilaumu, wako nishamchukua,
penzi ulimdhulumu, visa ukamfanyia,
chachandu vitamutamu, wala hukumpatia,
bwana akapata wazimu, kashindwa kuvumilia,
kwangu akatia timu, tiba nikampatia.
nikampa vitu adimu, kwako hajajionea,
amri akasalimu, magoti kunipigia,
huku akijilaumu, kwako kapotea njia,
mimi naletewa ndani, wewe watanga na njia,
Magomeni, Buguruni, ndala zakukatikia,
wasela wa vijiwani, nafuu wajipatia,
uroda kwa foleni, kwako wajipendelea,
wewe gumzo mjini, watu wanahadithia,
umeachika ndoani, kwa yako mbaya tabia,
unaogea jikoni, bafuni unapikia,
nampikia maandazi, na chai ya tangawizi we mwenzangu,
kisha natoa dozi, impayo usingizi we mwenzangu,
ohoo utalia, mwenzangu jiji utalijua.

Pamoja na ukweli kuwa haya yote yanasemwa kwa njia ya majigambo, yanatueleza sifa mbalimbali anazopaswa kuwa nazo mwanamke anayesawiriwa katika muziki wa *mipasho*.

Mwanamke mlinzi wa ndoa

Pamoja na kutumia mbinu mbalimbali za kumliwaza na kumridhisha mwanamume, mwanamke hutumia mbinu zingine, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha anawapasha ukweli wale wote wenye mwelekeo wa kumuwindi mume wake. Mbinu za kumdhoofisha adui, ambaye ni mwanamke anayetarajiwa kuwa mke mwenza au hawara wa mwanamume ni kupambana naye kwa maneno. Vita vya maneno vinavyojitokeza katika muktadha huu vina sifa kubwa ya kuwa na mwelekeo wa majigambo, ambapo mtambaji hujipa sifa kemkem na kuonyesha udhaifu mkubwa wa mshindani wake. Hata hivyo, majigambo ya aina hii kwa kiasi kikubwa ni yale yanayomweka mwanamume kama bwana wa kutumikiwa na wanawake. Kwa hiyo, wanawake hushindana, hutambiana, na kutukanana huku tambo na matusi hayo yakihusishwa na kufanikiwa au kushindwa kumridhisha au kumliwaza mwanamume. Ubeti ufuatao wa wimbo ukitwao *Huna Mpango* ulioimbwa na kikundi cha *Tanzania One Theatre (TOT)* unaonyesha mfano wa vita vya maneno, vijembe na kejeli vinavyorushwa kwa mwanamke anayeonekana kuwa na mwelekeo wa kumshawishi mume au hawara wa mwanamke mwingine.

TOFAUTI YA DHANA YA MWANAMKE

Huna mpango

kutaka bwana si wako, utaumia kwa sana,
kila mtu mke mwenzako, ukiamua kuchuna,
mimi si mgomvi wako, wala hatujafanana,
sikujui utokako, upo upo nakuona,
mwili ndo mtaji wako, msingi kuwa na bwana.

kutaka kula si vyako, utajiua mapema,
wengine mabosi wako, unaifuta heshima,
hata kwa rafiki zako, waramba huna noma,
hujui shemeji zako, we pesa ndo inasema,
vishawishi bodi lako, wala halijaundwa vyema.

Kwa hiyo, ili kuhakikisha kuwa mwanamume hashawishiwi na wanawake wengine, mwanamke anapaswa kuangalia nyendo za wanawake wengine kwa hawara yake au mumewe, na pale anapobaini nyendo hizo, anapaswa kuzizuia kwa kumpasha mwanamke anayetaka kumchukua hawara au mume wake kama tulivyoona katika baadhi ya tungo hapo juu.

Tofauti za dhana ya mwanamke katika ngoma ya *Mtuli* na *mipasho*

Kama tulivyoona hapo juu, kuna tofauti bayana kati ya dhana ya mwanamke katika muziki wa *mipasho* na ngoma ya *Mtuli*. Kwa ujumla, katika ngoma ya *Mtuli*, mwanamke ni mtu anayeongeza nguvukazi katika kaya na anapaswa kuwa mfano wa kufanya kazi. Halikadhalika, mwanamke hutegemewa katika kuiweka kaya katika hali nzuri kiuchumi na kijamii. Sifa kubwa miongoni mwa nyingi anazopaswa kuwa nazo mwanamke ni uwezo wa kufanya kazi. Aidha, suala la uzuri wa sura au maumbile yanayomsisimua mwanamume si kigezo muhimu cha kuolewa kama inavyojitokeza katika *mipasho*. Changamoto kubwa zinazowakabili wanawake kama wanavyosawiriwa na ngoma ya *Mtuli* ni kufanya kazi kwa bidii, kuwa na watoto, na kuwalea watoto kulingana na mila na desturi za Kibena.

Changamoto kubwa zinazojitokeza katika *mipasho* kama zilivyojadiliwa na wasanii kadhaa hapo juu ni uzuri, namna ya kumliwaza mwanamume na mbinu za kupambana na wanawake wengine ili wasiingilie himaya yake. Hata hivyo, pamoja na nyimbo nyingi za *mipasho* kuwa na mwelekeo huu, kuna baadhi ya nyimbo zinazosisitiza tabia njema kuwa ni kigezo muhimu kuliko sura. Mojawapo ya nyimbo hizo ni *Wasia* kama ulivyonukuliwa na Khamis (2004: 30):

Wasia

ichukue hii siri iwe kwako ni wasiya,
huwi katika wazuri ila kwa njema tabiya,
uwe mwenye kusubiri siivamie duniya.
kiitikio:
tabia kitu azizi kiumbe akiwa nayo,
si hoja sura nzuri na watu kukusifiya,
au umbo la fakhari mwenyewe kujivuniya,
huwi na nyingi jeuri hayo yakasaidiya.

ANGELUS MNENUKA

Kama jina la wimbo lilivyo, huu ni wasia unaotolewa kwa msichana au mwanamke yeyote. Tofauti na nyimbo zingine za *mipasho* zinazotokana na vijembe vyenye hisia za chuki na wivu ndani yake, wimbo huu unatoa wasia wa kweli na maadili ambayo kila mwanamke anapaswa kuwa nayo.

Mtazamo tuupatao katika *mipasho* ni kwamba mwanamke hafanyi kazi kubwa za uzalishaji mali, badala yake kazi hiyo hufanywa na mwanamume. Jukumu na wajibu mkubwa wa mwanamke ni kuitunza nyumba na kumwandalia mazingira mwanamume ili atokapo kutafuta chochote aone kila kitu kinapendeza ikiwa ni pamoja na mwanamke mwenyewe awe katika hali ya usafi na kumvutia mumewe. Kipande kifuatacho cha ubeti mmoja katika wimbo wa *Utalijua Jiji* unadokeza wazo hilo.

Utalijua jiji

nampikia maandazi, na chai ya tangawizi we mwenzangu,
kisha natoa dozi, impayo usingizi we mwenzangu,
ohoo utalia, mwenzangu jiji utalijua,
mwenzangu huna ujuzi, rudi tena kajifunze we mwenzangu,
ohoo utalia, mwenzangu jiji utalijua,
bibi acha upuuzi kuishi na mume kazi mwenzangu,
ohoo utalia, mwenzangu jiji utalijua,
mume ataka malezi, sio mambo ya kihuni we mwenzangu,
ohoo utalia, mwenzangu jiji utalijua,
ngebe na jhuri zako, leo zimekuishia we mwenzangu.

Dhana ya mwanamke, ambayo inahusishwa moja kwa moja na wajibu na majukumu ya mwanamke katika jamii inapaswa kutazamwa kwa kuihusisha na muktadha wa kijamii kwa sababu kuna uhusiano mkubwa wa kuathiriana baina ya sanaa na mazingira ambamo sanaa inayohusika inatendwa (Silbermann 1968). Tunapolinganisha *mipasho* na *Mtuli* tunalazimika kuihusisha wazo hilo pia ili mjadala wetu uwe na upeo mpana zaidi.

Kama tulivyosema hapo awali, utamaduni huathiriwa na tabia ya nchi, hali ya hewa na mazingira kwa ujumla. Vivyo hivyo, mgawanyo wa majukumu ambao humwingiza mwanamke katika wajibu na majukumu yake unaathiriwa na mambo hayo. Ili tuelewe vizuri uhusiano uliopo baina ya mazingira na utamaduni, tuangalie mfano ufuatao: wanawake wa Kiskimo waliweza kufikia hatua ya kuu mtoto wa kike bila ya kujisikia kuwa na hatia yoyote wala kuwajibika kijamii. Halikadhalika, wazee wasiokuwa na mchango katika jamii waliweza kuachwa wafe katika theluji. Kwa mujibu wa Rachels (2004), watu wengi wanaweza kufikiri kuwa Waeskimo ni watu wasio na maadili ya kiutu, hasa kuhusu umuhimu na thamani ya maisha, lakini sababu kubwa zilizowafanya Waeskimo wafanye matendo hayo yanayoonekana kuwa si ya kiutu ni mazingira magumu waliyonayo. Mazingira yao hufanya utafutaji wa chakula kuwa mgumu sana. Hali kadhalika, mwanamke aliweza kuu watoto wa kike kwa sababu wanaume ndio watafutaji wakubwa wa chakula, hivyo ni afadhali kuwa na watoto wengi wa kiume kuliko watoto wa kike. Katika mjadala wetu tunaona kuwa mila na desturi zinazomfanya mwanamke anayejadiliwa katika ushairi wa *mipasho* ndizo zinazomfanya mwanamke anayejadiliwa katika ushairi wa Kibena awe hivyo. Mazingira ya pwani ambayo

TOFAUTI YA DHANA YA MWANAMKE

huwafanya wanaume kuwa msingi wa familia na chanzo cha kipato kuliko wanawake ndicho kinachowafanya wanawake wa maeneo hayo kuwategemea wanaume na kuwanyenyekea kwa kiasi kikubwa. Yumkini mila na desturi ama za dini ya Kiislamu na tamaduni za Kiarabu, au vyote kwa pamoja vimeathiri mfumo wa maisha ya watu wa maeneo ya pwani ambapo wanawake huishi nyumbani huku wakiwategemea kwa kiasi kikubwa waume zao ili wawaletee chochote. Tunahusisha dini ya Kiislamu na utamaduni wa Kiarabu kwa sababu kwa miaka mingi wakazi wengi wa maeneo ya pwani ni Waislamu na wameathiriwa kwa kiasi kikubwa na utamaduni wa Kiarabu kutokana na kuishi na kushirikiana na Waarabu kwa karne nyingi. Jambo hili linatokana na Waarabu, ambao wengi wao ni Waislamu, kufika na kuishi katika maeneo ya upwa wa pwani ya Afrika Mashariki kati ya miaka 500–800 BK (Massamba 2002).¹⁵

Kwa upande mwingine, mazingira waishio Wabena yanaruhusu shughuli za kilimo kufanyika. Kilimo ni shughuli inayofanywa na kila mtu ikiwa ni pamoja na watoto, vijana na wazee. Kilimo ni chanzo cha chakula na kipato na vilevile ni kazi ngumu inayohitaji nguvu-kazi kubwa ili kulima eneo kubwa ambalo litatosheleza chakula kwa watu wengi. Kutokana na mazingira haya, mwanamke wa Kibena ana uwezo wa kujitafutia chakula na kipato bila msaada mkubwa kutoka kwa mwanamume. Mwanamke anayeishi katika mitara kwa mfano, ana uhuru zaidi na uwezo mkubwa wa kuitawala nyumba yake kuliko mwanamke aliye katika ndoa ya mume na mke mmoja kutokana na uwezo mkubwa wa kutoa uamuzi katika nyumba. Mwanamke anayeishi katika mitara hawezi kutegemea kipato kutoka kwa mumewe kwa sababu kuna wanawake wengi ambao hawawezi kumtegemea mwanamume mmoja ili kuwatimizia mahitaji yao hasa yale yanayoweza kutimizwa na wao wenyewe kama suala la upatikanaji wa chakula. Kutokana na mazingira hayo, kila mwanamke hujitegemea karibu kwa kila kitu.

Kwa hiyo, kutawala kwa wazo fulani katika maudhui ya kazi ya sanaa ya eneo fulani kuna-tegemeana sana na utamaduni ambao unatokana na tabia ya nchi, hali ya hewa na mazingira kama tulivyokwishasema hapo juu. Tunaweza kuliona wazo hilo pia katika kazi za fasihi za Kisomali, ambazo kutokana na kuishi katika mazingira ambamo ngamia ana umuhimu mkubwa sana katika maisha ya kila siku, kazi za fasihi za Kisomali zimesheheni sifa mbalimbali za mnyama huyo (Abokor 1986).

¹⁵ Kuna mambo mawili tofauti kabisa tunayopaswa kuyaweka bayana katika hoja hii. Kwanza, utamaduni wa mwanamke kubaki nyumbani, ambao ndio unaojadiliwa katika makala hii ni athari za Kiarabu au Kiislamu au vyote kwa pamoja. Pili, muziki wa *taarab* na *mipasho*, kujadili mada zinazohusu suala la wanawake kubaki nyumbani na wanaume kutegemewa kwa shughuli za kiuchumi. Utamaduni wa Kiarabu na dini ya Kiislamu vilikuja kivyao karne nyingi zilizopita, na muziki wa *taarab* uliozalisha *mipasho* ulikuja kivyake katika miaka ya 1880 kwa ushawishi wa Sultan Seyid Bargash (Askew 1997). Kwa kuwa sanaa hujadili masuala yanayozunguka jamii na kwa kuwa muziki wa *taarab* na *mipasho* umejikita sana katika maeneo ya Dar es Salaam na Zanzibar, yaliyoathiriwa na utamaduni tulioitaja hapo juu, muziki wa *taarab* na *mipasho* hujadili masuala hayo ya mwanamume kutegemewa na mwanamke katika shughuli za kiuchumi. Kutokana na tofauti hiyo, si jambo la ajabu kuona muziki wa *mipasho* ukienda kinyume kabisa na tamaduni za Kiarabu na dini ya Kiislamu (Traoré 2007, Ntarangwi 2003).

Ingawa suala la mitara linajitokeza katika jamii zote zinazosawiriwa na nyimbo kutoka katika pande zote zilizojadiliwa hapo juu, bado suala hili linasababishwa na sababu tofauti kama ilivyodokezwa hapo juu. Ndoa za mitara zinajitokeza katika jamii iliyosawiriwa na nyimbo za Kibena tunaweza kusema zinatokana na haja ya mwanamume kupata mtoto ikiwa mke wake anafikiriwa kuwa ndiye kikwazo kikubwa katika upatikanaji wa mtoto kama ilivyo kwa jamii nyingi za Kiafrika (Mbiti, ameshatajwa). Vilevile, ndoa za mitara zinasababishwa na mahitaji ya mwanamume wa kijijini ambayo ni kuridhisha tamaa zake, au wakati mwingine kuepukana na makatazo ya kitamaduni kama vile kutokufanya tendo la ngono na mwanamke anayenyonyesha, vilevile, inawezekana pia wazo la kuingia katika mitara linatokana na uzee, ugonjwa au kutovutia kwa mke wa awali (Shorter 1998). Kuoa wake wengi ni sifa kwa mwanamume iwapo ana uwezo wa kufanya hivyo. Wazo hilo linadokezwa katika wimbo ufuatao wa Kibena:

Samba ya Efa

*samba ya Efa ilima nani?
ndilima yune ni telekita yangu. (2)*

*Swaa!¹⁶ ng'wale, swaa! ng'wale,
Swaa! ng'wale, pa mgunda gwangu. (2)*

Shamba ya Efa

*shamba ya Efa, atalima nani?
nitalima mimi mwenyewe kwa
trekta langu. (2)*

*Swaa! kwale, swaa! kwale,
Swaa! kwale shambani pangu. (2)*

Wimbo huu, kama zilivyo zingine hapo juu, huimbwa katika matukio ya harusi. Tofauti na nyimbo zingine, katika wimbo huu tunasikia sauti ya mwanamume anayejigamba kuwa yeye ndiye anayeweza kumwoa msichana aitwaye Efa. Mwanamume huyu anadhihirisha uwezo wake kwa kuwafukuza wanaume wengine, ambao katika wimbo huu imetumika lugha ya picha *kwere*.

Tunaweza kusema kuwa mitara inayojitokeza katika jamii inayosawiriwa na muziki wa *mipasho* inatokana na mashindano ya wanawake kumpata mume mmoja ili kukidhi mahitaji yao. Mashindano hayo huendelea kwa wanawake (wake au mahawara) kushindana kumliwaza na kumpendezesha mume ili kila mmoja aonekane ni mwanamke bora kuliko wengine. Haya tunayapata kutokana na desturi ya kupigana vijembe vinavyowahusu wanawake ambao wana-dhalilishana kwa sababu ya mwanamume. Ubeti ufuatao wa wimbo wa *Tutabanana Hapahapa* kama ulivyonukuliwa na Traoré (2004: 78) unadokeza wazo hilo:

Tutabanana hapahapa

*tutabanana hapa hapa nakwenda nawe sambamba,
kama wewe wa nyumba kubwa na mimi wa nyumba ndogo,
sote wa mume mmoja sote tuna haki sawa,
usilete za kuleta kunitimua huwezi,
sinifikiri goi goi mimi niko fiti kishenzi,
tutabanana hapahapa tule mkono kwa mkono,
ukishindwa shauri yako ukisusa hiyari yako.*

¹⁶ “swaa!” ni sauti itumiwayo na watu wa jamii ya Kibena kufukuza wanyama na ndege waharibifu katika mashamba yao.

TOFAUTI YA DHANA YA MWANAMKE

Katika ubeti huo tunaona maneno yanayotolewa na mwanamke ambaye anaonekana ni mke wa pili dhidi ya mwenzake aliyetangulia kuolewa yana hisia za chuki kati ya mke wa kwanza na mke wa pili ambao wote kwa pamoja wanashindana katika kumridhisha mwanamume ili ampende zaidi mmoja wao.

Tofauti nyingine inayojitokeza katika jamii hizi mbili ni ile inayohusu mfumo wa uzalishaji mali. Jamii ya Kibena, kama tulivyosema hapo juu, ni jamii ya wakulima, ambapo karibu kila mtu hujishughulisha na kilimo. Katika shughuli hii, wanawake, kama ilivyokwishadokezwa, ni sehemu ya nguvukazi. Suala hili haliihusu jamii ya Kibena pekee bali ni hulka ya jamii ambazo kilimo kwao ni shughuli muhimu. Jamii nyingi za wakulima katika bara la Afrika na Asia zinafanana kitabia hasa kwa wanawake kujishughulisha kwa kiasi kikubwa katika shughuli za kilimo (Ogunlela na Mukhtar 2009, Mwaipopo 1995).

Kwa upande mwingine, jamii za maeneo ya pwani, kutokana na sababu za kihistoria, na kukomaa kwa mfumo wa kimwinyi, ambapo mwanamke hupaswa kumnyenyekea mwanamume, sambamba na mwanamke kufanywa kama chombo ambacho mamwinyi hukitumia kwa kujiliwaza, nafasi ya mwanamke imekuwa ni kujiweka chini ya mwanamume kwa kujitahidi kumfurahisha na kumliwaza. Mfano mojawapo unaodokeza vizuri wazo hili ni baadhi ya beti katika *Utenzi wa Mwanakupona* zinazosisitiza utii kwa mwanamume.¹⁷ Kwa mujibu wa utenzi huu, nyingi kati ya mbinu anazopaswa mwanamke kuzitumia anapoishi na mwanamume ni kumkweza mwanamume (Mulokozi 1999). Mfano ufuatao ni baadhi tu ya beti zinazotoa mwongozo wa namna ya kumfanyia mwanamume.

31. kilala siikukuse
mwegeme umpapase
na upepo asikose
mtu wa kumpepea.

32. kivikia simwondoe
wala sinene kwa yowe
keti papo siinue
chamka kakuzengea.¹⁸

Beti hizi zinaonesha utamaduni na nafasi ya mwanamke katika jamii za kimwinyi. Kwa hiyo, dhana ya mwanamke katika muziki wa *taarab* (*mipasho*) haijaibuka hivi karibuni, ni dhana yenye mizizi mirefu iliyotokana na sababu nyingi, baadhi yake ni sababu za kimfumo katika maeneo ya pwani ya Afrika Mashariki.

Kufanana kwa baadhi ya vipengele

Pamoja na usawiri huo wa dhana ya mwanamke, ieleweke kwamba muziki wa *taarab* unajadili masuala mengi yanayomzunguka mwanajamii, hususani anayeishi maeneo ambamo muzi-

¹⁷ Wazo hili limefafanuliwa na Khatib (1985), Senkoro (1988) na El-Maawy (2011). Pamoja na kupingwa na Njozi (1990), mawazo haya bado yana mashiko kwa kiasi kikubwa hasa tukiangalia namna mawazo yenye mwelekeo huohuo yanavyoibuliwa katika *mipasho*. Kwa mfano, Khatib (ameshatajwa) anasisitiza kuwa, “Tungo hii ya Mwanakupona ni zao la fasihi ya kimwambao iliyorithiwa na kupata utomvu wa uhai wake kutokana na utamaduni ulioghoshiwa na maadili ya Kiislamu katika karne ya kumi na tisa.” (uk. 46).

¹⁸ Mulokozi (1999: 128) aliyehariri utenzi huu amefafanua baadhi ya maneno magumu katika utenzi huu kama ifuatavyo: *siikukuse* maana yake “usijitenge”, *mwegeme* maana yake “mkaribie”, *kivikia* maana yake “akianza kusinzia”, *kakuzengea* maana yake “akakutafuta”.

ANGELUS MNENUKA

ki huu umetawala. Baadhi ya masuala hayo ni kufuata maadili ya dini, kazi, mapenzi, siasa, na uhusiano kati ya wanajamii kwa ujumla. Kwa mfano, kuna nyimbo mbalimbali za *taarab* zinazoimbwa na wanaume zikiwasifia wapenzi wao wa kike na kuwapiga vijembe wanawake wengine wenye nia ya kutaka kuvuruga penzi hilo. Vilevile kuna nyimbo zinazohamasisha kufanya kazi kama moja ya majukumu makubwa katika jamii. Ubeti ufuatao wa *Dunia ni Pesa* unaonyesha kuwa pamoja na masuala yaliyojadiliwa hapo juu, *mipasho* ina baadhi ya nyimbo zinazohamasisha watu kufanya kazi.

Dunia pesa

fanya kazi upate pesa,
jishughulisha ujenge maisha,
kwani kila mtu ana riziki yake,
ujue Mungu hamtupi mja wake
kikubwa kidogo, akiba uweke
jua akiba ina faida yake.

Ubeti huo unatoa picha ya mafunzo na busara zilizomo katika muziki wa *mipasho* na kuwa suala la kazi halijasahuliwa kabisa katika muziki huu. Bila shaka ubeti huu unadokeza kuwa pamoja na mfumo wa jamii za watu wa maeneo ya pwani kutawaliwa na desturi za wanaume, wanawake wana nafasi kubwa ya kujishughulisha katika shughuli zinazowaingizia kipato. Ubeti huo unasisitiza kuwa hata kidogo kinachopatikana baada ya kufanya kazi ni vizuri kihifadhiwe kama akiba kwa sababu akiba ina umuhimu mkubwa katika maisha ya binadamu.

Kwa upande mwingine, tukiichukulia dhana ya *mipasho* kama ilivyoelezwa hapo juu, kuwa ni “kumweleza mtu ukweli”, katika ngoma ya *Mtuli* kuna nyimbo zinazoimbwa kwa namna ileile ya kumweleza mtu ukweli. Tofauti kubwa inayojitokeza ni umuhimu wa suala husika katika jamii. Jamii ya Kibena, kama zilivyo jamii nyingi za Kibantu, huamini katika dhana ya uchawi¹⁹. Kwa kawaida, Wabena huamini mchawi ana uwezo wa kutoa uhai wa mtu mwingine. Kutokana na suala hilo kutowapendeza watu wengi katika jamii yao, kuna nyimbo nyingi zinazoonyesha ubaya wa matendo ya aina hiyo.

Katika nyimbo za kumbukumbu za marehemu na matukio yanayoendana na hayo, kuna nyimbo ambazo kitabia zinaweza kufanana na *mipasho* kama tulivyosema hapo juu ambapo mchawi hutajwa na kuimbwa waziwazi ili aachane na matendo hayo yasiyovumiliwa katika jamii. Ubeti ufuatao wa wimbo wa *Uwii*²⁰ unamtaja mhusika anayedhaniwa kuwa ni mchawi aliyemroga mtoto.

¹⁹ Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI 2004), dhana ya uchawi inahusisha matumizi ya dawa au vitabu vya kichawi kwa malengo ya kuleta madhara kwa viumbe; sihiri, juju, machezo. Katika makala hii, tutatumia dhana ya uchawi kama matendo au mbinu zozote aghalabu za kijadi zitumiwazo na mtu ili kumdhuru mtu - au kikundi cha watu - kwa sababu fulani.

²⁰ Hii ni sauti ya kilio inayoashiria mara nyingi kuwa kuna tatizo, si sauti inayopaswa kutolewa kiholela.

TOFAUTI YA DHANA YA MWANAMKE

Uwii

*Uwii Muhimba,²¹
Uwii Muhimba,
Uwii Muhimba,
kana ka vene lelo tuwene!*

Uwii

Uwii Muhimba,
Uwii Muhimba,
Uwii Muhimba,
mtoto wa watu leo tumeona!²²

Wimbo wenye ubeti huo ni miongoni mwa nyimbo zenye tabia ya *mipasho*, yaani kuwaeleza watu ukweli bila kuficha ili waache mienendo isiyokubalika katika jamii.

Hitimisho

Mwanamke wa Kitanzania, na wa Kiafrika kwa ujumla, ana sura changamani mno kiasi cha kutoweza kumfasili na kumchambua kirahisi kama wengi wanavyodhani. Katika nchi ya Tanzania kwa mfano, kuna jamii mbalimbali zenye mila na desturi zinazotofautiana kwa kiwango kikubwa. Wajibu na majukumu ya mwanamke katika jamii hizo hutofautiana kwa viwango mbalimbali pia. Kwa hiyo, ni mtazamo potofu kudhani kuwa wanawake wa Kitanzania wanakabiliwa na changamoto za aina moja.

Katika tungo mbalimbali tulizozichambua katika makala hii tumeona kuwa changamoto kubwa ya mwanamke anayesawiriwa katika *mipasho* ni kumtegemea na kumnyenyekea mwanamume. Tofauti na changamoto zinazomkabili mwanamke anayesawiriwa katika *mipasho*, mwanamke anayesawiriwa katika ngoma ya *Mtuli* katika jamii ya Wabena anakabiliwa na changamoto ya kuzidiwa na kazi na wala si kumtegemea mwanamume kwa kiwango kikubwa. Kwa hiyo, mwanamke wa Kibena anakabiliwa na changamoto ya kupata msaada kutoka kwa mwanamume ili apate unafuu wa kazi na kupata nafasi ya kuwalea watoto. Mwanamke anayesawiriwa katika *mipasho* anahitaji kusaidiwa ili ajitegemee, na njia pekee ya kumsaidia mwanamke huyu ni kumjengea mazingira yatakayomfanya ajitegemee.

Dhana za ujumi zinategemeana sana na muktadha wa kimazingira. Kwa mfano, kwa Wabena kama inavyodokezwa katika tungo zao, mwanamke anayestahili kuolewa ni yule mwenye bidii ya kazi na tabia njema bila kujali sana uzuri wa sura au maumbile yake. Hatuwezi kudai moja kwa moja kuwa mwanamume wa Kibena hana vionjo au utambuzi wa uzuri wa sura au maumbile ya mwanamke, la hasha! Tunalosisitiza hapa ni kwamba, pamoja na uzuri wa sura na maumbile ya kuvutia, mwanamke anapaswa kuwa na sifa za msingi; mojawapo ikiwa ni bidii ya kazi.

Uzuri pekee hauwezi kuwa kigezo cha mwanamume kumwoa mwanamke katika jamii asilia ya Kibena. Kwa hiyo, miito inayotolewa na mashirika mbalimbali ya kitaifa na kima-

²¹ Hili ni jina la mtu anayeaminiwa kuwa ni mchawi, kwa hiyo, jina la mtu yeyote anayedhaniwa kuwa ni mchawi linaweza kupachikwa hapo.

²² Maana ya neno “kujionea” limebeba dhana pana zaidi. Katika muktadha huu limetumika “tumethibitisha” au “tumegundua”, ikimaanisha kwamba tangu mtoto huyo alipokumbwa na matatizo hawakujua chanzo ni nini lakini sasa wamegundua kuwa chanzo ni huyo mchawi anayelitwa Muhimba. Ndiyo maana wimbo huu unaanza na sauti ya kilio dhidi ya mchawi anayetajwa.

taifa kwa wanawake kujitegemea ili wawe na uhuru zaidi, ni miito inayowa baadhi tu ya wanawake na sio wote, kwa sababu kwa baadhi ya wanawake kujitegemea sio suala la kuambiwa leo hii, ni suala lililokuwemo kwenye jamii miaka nenda rudi.

Marejeo

- Abokor, A. C. 1986. *The Camel in Somali Oral Traditions*. Uppsala: Somali Academy of Sciences and Arts and the Scandinavian Institute of African Studies.
- Askew, K. M. 1997. *Performing the Nation: Swahili Music and Cultural Politics in Tanzania*. Chicago and London: University of Chicago Press.
- BAKIZA. 2010. *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.
- Balogun, O. A. 2010. Proverbial Oppression of Women in Yoruba African Culture: A Philosophical Overview. *Thought and Practice: A Journal of the Philosophical Association of Kenya (PAK.) New Series 2*, 1: 21-36.
- Beez, J. & S. Kolbusa. 2003. Kibiriti Ngoma: Gender Relations in Swahili Comics and Taarab-music. *Stichproben. Wiener Zeitschrift für kritische Afrikastudien 5*, 3: 50-71.
- Chaula, E. H. Y. 1989. *Aspects of Ki-Bena Phonology: The Case of Kimavemba Variety*. Tansifu ya MA isiyochapishwa. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Culwick, A. T. & G. M. Culwick. 1935. *Ubena of the Rivers*. London: George Allen & Unwin Ltd.
- El-Maawy, A. A. A. 2011. *Jawabu la Mwana Kupona: Mausiyo ya Mke wa Kisasa, na Wasiya wa Mwana Kupona*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.
- Finnegan, R. 1976. *Oral Poetry: Its Nature, Significance and Social Context*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Finnegan, R. 1970. *Oral Literature in Africa*. Oxford: Clarendon Press.
- Igobwa, E. S. 2007. Taarab and Chakacha in East Africa: Transformation, Appreciation and Adaptation of Two Popular Music Genres of the Kenyan Coast. *Conference on Music in the World of Islam – Assialh 8-13 August*: 1-8.
- Karbusicky, V. 1968. The Interaction between 'Reality-Work of Art-Society'. *International Social Science Journal: The Arts in Society XX*, 4: 644-666.
- Khamis, S. A. M. 2005. Clash of Interests and Conceptualisation of Taarab in East Africa. *Swahili Forum XII*: 133-159.
- Khamis, S. A. M. 2004. Images of Love in the Swahili Taarab Lyric: Local Aspects and Global Influence. *Nordic Journal of African Studies 13*, 1: 30-64.

TOFAUTI YA DHANA YA MWANAMKE

- Khamis, S. A. M. 2002. Wondering about Change: The Taarab Lyric and Global Openness. *Nordic Journal of African Studies* 11, 2: 198-205.
- Khatib, M. S. 1985. Utenzi wa Mwanakupona. *Mulika* 17: 46-52.
- Kirkegaard, A. 2002. "Tranzania" - A Cross-Over from Norwegian Techno to Tanzanian Taarab. *Playing with Identities in Contemporary Music in Africa*, ed. by Palmberg, M. & A. Kirkegaard. Uppsala: Nordiska Afrikainstitutet and the Sibelius Museum/Department of Musicology Åbo Akademi University. Pp. 46-59.
- Magesa, L. 1998. *African Religion: The Moral Traditions of Abundant Life*. Nairobi: Paulines Publications Africa.
- Massamba, D. P. B. 2002. *Historia ya Kiswahili: 50 BK hadi 1500 BK*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Mbiti, J. S. 1969. *African Religions and Philosophy*. London: Heinemann.
- Mnenuka, A. 2009. *Reiteration in Bena Songs and Folktales: A Comparative Approach*. Tasnifu ya MA (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mulokozi, M. M. (ed.) 1999. *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mumford, B. W. 1934. The Hehe-Bena-Sangu Peoples of East Africa. *American Anthropologist, New Series* 36, 2: 203-222.
- Mwaipopo, R. 1995. Gender Issues in Agriculture in Tanzania: An Overview. *Gender and Development in Tanzania: Past, Present and Future*, ed. by Njau, Adela E. & T. Mruma. Dar es Salaam: Women Research and Documentation Project. Pp. 205-215.
- Njozi, H. M. 1990. Utendi wa Mwanakupona and Reception Aesthetics. *Kiswahili. Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahil -*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam 57: 55-67.
- Ntarangwi, Mwenda. 2003. *Gender, Performance and Identity: Understanding Swahili Culture realities through Songs*. Trenton, Asmara: Africa World Press.
- Okpewho, I. 1992. *African Oral Literature: Background, Character, and Continuity*. Bloomington, Indianapolis: Indiana University Press.
- Ogunlela, Y. I. & A. A. Mukhtar. 2009. Gender Issues in Agriculture and Rural Development in Nigeria: The Role of Women. *Humanity & Social Sciences Journal* 4, 1: 19-30.
- Rachels, J. 2004. The Challenge of Cultural Relativism. *Fifty Readings in Philosophy Second Edition*, ed. by D. C. Abel. New York: McGraw Hill. Pp. 395-407.
- Scheub, H. 1985. A Review of African Oral Traditions and Literature. *African Studies Review* 28, 2/3: 1-72.
- Senkoro, F. E. M. K. 1988. *Ushairi: Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: DUP.

ANGELUS MNENUKA

- Shorter, A. 1998. *African Culture: An Overview*. Nairobi: Paulines Publications Africa.
- Silbermann, A. 1968. Introduction: A Definition of the Sociology of Art. *International Social Science Journal: The Arts in Society* XX: 567-588.
- Traoré, F. A. 2007. Women's Taarab Lyrics in Contemporary Zanzibar. *Swahili Forum* 14: 181-195.
- Traoré, F. A. 2004. Continuity and Change in Zanzibar Taarab Performance and Poetry. *Swahili Forum* 11: 75-81.
- TUKI. 2004. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- Vázquez, A. S. 1973. *Art and Society: Essays in Marxist Aesthetics*. London: Merlin Press.